# TATHMINI YA TAFSIRI YA JALADA LA KITABU: MIFANO KUTOKA TAFSIRI YA *THE BLACK HERMIT* (THIONG`O, 1968) NA *KIFO KISIMANI* (MBERIA, 2001)

*Haule Jacob*

**Ikisiri**

*Lengo kuu la tafsiri ni kufanikisha mawasiliano kwa sababu hadhira lengwa haijui lugha wala utamaduni chanzi. Hivyo, mfasiri anapaswa kuwa mwaminifu kwa kulinda ukweli na ufasaha wa ujumbe wa matini chanzi katika matini lengwa. Ujumbe huo hubebwa na vipashio mbalimbali (maneno, virai, sentensi na aya) ambavyo mfasiri hana budi kuvizingatia. Aidha, mfasiri huzingatia vipengele vya lugha na masilugha vilivyomo katika jalada la tafsiri ili aweze kuandaa jalada la matini lengwa linaloendana na ujumbe wa jalada la matini chanzi. Hii ni kwa sababu jalada hubeba maana na ujumbe ulio kamili kwa kutumia lugha na masilugha. Hivyo basi, makala hii imetathmini tafsiri ya jalada la tafsiri ya tamthiliya ya The Black Hermit iliyoandikwa na Ngugi wa Thiong`o (1968), kisha ikatafsiriwa kama Mtawa Mweusi na Ngugi wa Thiong`o (1970) na tamthiliya ya Kifo Kisimani iliyoandikwa na Kithaka wa Mberia (2001) na ikatafsiriwa kama Death at the Well na Khalfan Kasu (2011). Tathmini imefanywa kwa kuchunguza kufanana na kutofautiana kwa tafsiri za majalada kati ya matini chanzi na matini lengwa. Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Usawe wa Kidhima iliyoasisiwa na Nida (1964). Data imekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji matini. Uchambuzi wa data hiyo umetumia mbinu linganishi na mkabala wa kitaamuli. Hatimaye, makala imebaini kuwa, licha ya vipengele kadhaa kufanana, bado kuna tofauti zinazojitokeza katika tafsiri hizo. Jambo hili linasababisha kutowiana kwa baadhi ya maudhui ya MC na ML. Hivyo, makala inapendekeza kwamba si kila jalada lazima litafsiriwe. Kutafsiriwa ama kutotafsiriwa kwa jalada la kitabu kunategemea muktadha wa tafsiri husika.*

## Utangulizi

Tafsiri ni jaribio la kuwasilisha ujumbe uleule ulioandikwa katika lugha moja kwa lugha nyingine (Kihore, 2005). Hii ina maana kuwa mawazo yaliyo katika matini chanzi yanaelezwa kimaandishi katika matini lengwa kwa kutumia lugha lengwa. Kwa upande wao, Mwansoko na wenzake (2015) wanaeleza kuwa tafsiri ni zoezi la

uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Changamoto ya fasili hii ni kwamba inajiegemeza zaidi katika maandishi pekee kama ilivyo kwa fasili ya Kihore (2005). Kwa muda mrefu, dhana ya 'tafsiri' imekuwa ikifasiliwa kwa kuhusisha maandishi pekee. Mwansoko na wenzake (2015) wanashadidia jambo hili kwa kusema kuwa mawazo yanayoshughulikiwa katika tafsiri sharti yawe katika maandishi, na si vinginevyo.

Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hivi sasa tunaona kuwa, tafsiri inaweza kuhusisha lugha ya maandishi na mazungumzo (Matkivska, 2014). Mathalani, matini chanzi (kuanzia sasa, MC) inaweza kuwa katika mfumo wa mazungumzo yaliyo katika sauti pekee au sauti na video na matini lengwa (kuanzia sasa, ML) ikawa katika mfumo wa video yenye maandishi ndani yake ambayo ndiyo tafsiri ya kisemwacho katika mazungumzo au video husika. Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa tafsiri ni mchakato wa uhawilishaji wa mawazo na ujumbe kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa ambapo mchakato huu unaweza kuhusisha lugha ya maandishi pekee au kutoka lugha ya mazungumzo kwenda katika maandishi.

Katika mchakato wa kutafsiri, mfasiri huzingatia vipashio mbalimbali vinavyounda MC. Vipashio hivyo ni kama vile maneno, virai, vishazi, sentensi, aya, na matini nzima. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa matini huweza kuambatana na vipengele kadhaa visivyo vya lugha. Vipengele hivi huweza kuwa na athari za moja kwa moja katika ujumbe wa matini husika. Vipengele hivyo ni kama vile picha, michoro, rangi, na alama mbalimbali. Waandishi hutumia vitu hivyo kama sehemu ya ubunifu wao ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Hivyo, ni lazima mfasiri azingatie vipengele hivyo anapotafsiri matini, hasa matini za kifasihi kwa kuwa hutumia ubunifu mkubwa.

Hivyo, makala hii imetathmini kazi mbili za tafsiri: Mosi, tamthiliya ya *The Black Hermit* iliyoandikwa na Ngugi wa Thiong`o (1968) na kutafsiriwa kama *Mtawa Mweusi* na Ngugi wa Thiong'o (1970). Pili, tamthiliya ya *Kifo Kisimani* iliyoandikwa na Kithaka wa Mberia (2001) na kutafsiriwa kama *Death at the Well* na Khalfan Kasu (2011).

## Nadharia ya Utafiti na Mbinu ya Uchambuzi wa Data

Tathmini hii imeongozwa na Nadharia ya Usawe wa Kidhima iliyoasisiwa na Nida (1964). Lengo kuu la nadharia hii ni kujaribu kupunguza tofauti zilizopo kati ya utamaduni na isimu katika tafsiri. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba kazi ya tafsiri lazima isababishe athari sawa kwa hadhira ya ML kama ilivyo katika MC. Yaani, inachokipata hadhira chanzi kiwe sawa na itakachokipata hadhira lengwa.

Hivyo basi, mawazo ya nadharia hii ndiyo yaliyoongoza mwelekeo wa makala hii. Msingi mkuu wa makala umeegemezwa katika uendanifu wa kidhima wa jalada la MC na jalada la ML. Kuendana au kutofautiana kati ya MC na ML ndiko kunakosababisha kuendana au kutofautiana kwa athari za matini husika kwa hadhira ya MC na ML kama nadharia hii inavyofafanua. Pia, data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji matini, ambapo majalada ya vitabu teule yalichunguzwa. Mintarafu uchambuzi wa data, mkabala wa kitaamuli umetumika kwa kuwa maelezo yametumika kujenga na kushadidia hoja mbalimbali.

**Jalada la Kitabu katika Tafsiri**

Dhana ya jalada la kitabu limejadiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwao ni TUKI (2013), Drew na Sternberger (2005) na Lyons (2017). Jalada ni karatasi ngumu inayofunika kitabu ambapo jina la kitabu huandikwa (TUKI, 2013). Matini nyingi, hasa zilizo katika muundo wa vitabu, huwa na majalada yake. Mwandishi wa MC hutumia ubunifu wake katika kuweka vitu mbalimbali katika jalada la kitabu ili kuleta mvuto wa kazi yake kwa wasomaji. Aidha, taarifa zilizomo katika jalada la kitabu hutoa taswira ya maudhui ya kitabu husika. Ndiyo maana, Drew na Sternberger (2005) wanasema kuwa jalada la kitabu ndilo linalotoa mawasiliano ya kwanza kati ya msomaji na kitabu husika. Majalada hayo hujumuisha taarifa kama vile jina la kitabu, jina la mwandishi, rangi mbalimbali, alama tofautitofauti, maelezo mafupi kuhusu kitabu, pamoja na picha mbalimbali zenye kung`aa ili kuvuta makini ya msomaji (Lyons, 2017). Jalada la kitabu huweza kuwakilisha sura za kitabu, aya, wahusika, matukio, mandhari, na maudhui ya kitabu katika picha moja. Jambo hili hufanya jalada la kitabu litoe taswira ya matini nzima.

Vilevile, wachapishaji wa vitabu huona kuwa vitabu ni bidhaa zinazopaswa kutangazwa na kuuzwa. Hivyo, huyaunda majalada ya vitabu vyao kwa ubunifu mkubwa ili viwe na mvuto kwa wasomaji kwa lengo la kuwavutia ili waweze kuvinunua. Hivyo basi, ni dhahiri kuwa jalada la kitabu hutengenezwa kwa ubunifu na hutoa taswira ya maudhui yaliyomo ndani ya kitabu husika. Kwa hiyo, taarifa zinazopatikana katika jalada la kitabu hazina budi kutiliwa maanani na wafasiri bila kujali kuwa ni lugha au masilugha. Mwandishi wa MC hutumia ubunifu wake kwa kutumia lugha na masilugha si tu kwa ajili ya kuvutia makini ya msomaji pekee, bali vitu hivyo huwa taswira ya maudhui ya matini nzima.

Vipengele vya lugha vinavyopatikana katika jalada la kitabu ni pamoja na jina la kitabu, na jina la mwandishi. Kwa upande mwingine ~~wa~~ vipengele vya masilugha ni pamoja na alama, rangi, picha, na michoro. Vipengele vya lugha na masilugha kwa pamoja hujenga taswira ya maudhui ya matini husika. Imekuwa kawaida kuona baadhi ya vipengele vya lugha vilivyomo katika jalada la kitabu, kama vile jina la kitabu, vikitafsiriwa na wafasiri mbalimbali. Hata hivyo, jambo la kujiuliza ni


kwamba, je, vipengele vya masilugha ni lazima vitafsiriwe? Je, ikibidi kuvitafsiri, vitafsiriwe kwa namna gani? Je, vikiachwa kuna athari gani zitakazojitokeza? Maswali haya ni muhimu kuyatafakari kwa kuwa huenda yakawakanganya wafasiri. Kwa mfano, mfasiri anapokutana na jalada lenye picha ya mtu au mnyama, je, atatafsiri vipi picha hiyo? Au aihamishe kama ilivyo na kuitumia katika ML? Akifanya hivyo, kutakuwa na athari gani za uelewekaji wa ujumbe wa MC kwa hadhira lengwa? Je, kutakuwa na uwiano wa kimaudhui kati ya jalada la MC na ML?


Sambamba na maswali hayo, jalada la kitabu ni kitu cha kwanza ambacho msomaji wa ML hukiona na humjengea picha ya muda mrefu akilini mwake. Hii ni kwa sababu ubongo wa binadamu huweza kung`amua haraka picha kuliko maneno (Coker, 2014). Ndiyo maana, Coker (keshatajwa) anafafanua kuwa, mtu anapoona picha (ya kwenye jalada) hupata ujumbe wa yaliyomo katika kitabu. Anaendelea kusema kuwa, picha iliyomo katika jalada la kitabu ni muhimu kuliko hata jina la kitabu au jina la mwandishi. Kwa hiyo, jalada bora humsaidia msomaji kutambua kuwa matini husika inamhusu au la.

Kadhalika, wataalamu mbalimbali wamejaribu kufafanua suala la tafsiri ya jalada la kazi ya tafsiri. Miongoni mwao ni Mossop (2018) aliyefanya tathmini ya ubora wa tafsiri kutoka lugha ya Kifaransa – Kiingereza kwa kutumia majalada ya kazi husika. Katika utafiti huo, amebaini kuwa kuna tofauti zinazojitokeza kati ya majalada ya tafsiri hizo, kiasi cha kusababisha kutowiana kwa maudhui ya MC na ML. Utafiti wa Mossop (2018) unatusaidia kufahamu changamoto za tafsiri ya jalada la tafsiri pamoja na athari zake. Hata hivyo, jambo hili amelishughulikia katika muktadha wa tafsiri ya Kifaransa-Kiingereza ingawa linajitokeza katika muktadha wa tafsiri za Kiswahili-Kiingereza. Ni dhahiri kuwa, hata wafasiri wa kazi za tafsiri zinazohusu lugha ya Kiswahili na Kiingereza wanakumbwa na changamoto ya tafsiri ya jalada la tafsiri.

## Tathmini ya Tafsiri ya Jalada la Kitabu

Makala hii imetathmini namna tafsiri ya majalada ya vitabu inavyofanywa na wafasiri katika tafsiri. Tathmini hii imejumuisha vipengele vinavyounda jalada la kitabu, yaani lugha na masilugha. Vilevile, tathmini hii imefanywa katika kazi mbili za tafsiri ambazo ni matini za kifasihi. Uteuzi wa tafsiri za kifasihi unatokana na ukweli kwamba matini hizi hutumia sanaa ya hali ya juu katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kuliko matini zisizo za kifasihi. Kazi zilizotathminiwa ni tafsiri ya tamthiliya ya *The Black Hermit* (*Mtawa Mweusi*) na *Kifo Kisimani* (Death at the Well). Kwa kuanza na tafsiri ya tamthiliya ya *The Black Hermit (Mtawa Mweusi),* kuna mambo kadhaa yanajitokeza kuhusu tafsiri ya jalada la kitabu:




Jambo la kwanza ni tafsiri ya jina la kitabu. Jina la kitabu, *The Black Hermit*, katika MC limetafsiriwa kama *Mtawa Mweusi* katika ML. Tafsiri hii inasadifu yaliyomo ndani ya kitabu kwa sababu mhusika Remi katika matini zote ana sifa zinazofanana. Hata hivyo, kuna tofauti ya kimaandishi kati ya MC na ML. Jina lililopo katika jalada la ML limekozwa zaidi kuliko la kwenye jalada la MC. Aidha, katika MC, jina la kitabu limeanza kuandikwa kabla ya jina la mwandishi. Mambo haya yanaweza kuwa na athari za kimawasiliano. Hii ni kwa sababu kitu chenye umuhimu zaidi ndicho huonekana mwanzoni na kukoza wino maandishi huweka msisitizo wa umuhimu wa kilichoandikwa (Macaya na Perea, 2014).

Jambo la pili ni tafsiri ya jina la mwandishi. Katika MC jina la mwandishi, limeandikwa tofauti na ML. Katika MC jina lina alama mbili za wimbi juu ilhali katika ML hakuna alama hizo. Tofauti hii inaweza kumfanya msomaji wa ML aliyebahatika kuiona MC kudhani kuwa labda ni waandishi wawili tofauti, ilihali ni mwandishi mmoja. Ikumbukwe kwamba, kuna uhusiano mkubwa baina ya jina, hisia na utambulisho wa mtu (Benedicta, 2012). Hivyo, jina la mwandishi inafaa liandikwe vyema na kwa namna isiyokanganya hadhira.

Jambo la tatu ni tafsiri ya picha ya mwenge. Katika MC kuna picha ya mwenge ulioshikwa na mtu katika mkono wake wa kuume na ameunyanyua juu. Mwenge huashiria uhuru au ukombozi katika jamii. Mhusika Remi (katika MC) ndiye anayeonekana kuwa tegemeo la wengi katika kuleta ukombozi wa jamii yake, na ndiye aliyeshika mwenge. Lakini, katika ML picha ya mwenge haipo kabisa, lakini kuna neno 'UHURU'. Kwa kuwa mwenge ni ishara ya uhuru, basi matumizi ya neno 'UHURU' katika ML badala ya picha yanaweza kuleta athari sawa za kiujumbe. Hata hivyo, jambo la kujiuliza ni kwamba, kwa nini katika MC mtu ashike mwenge na katika ML mtu haonekani kuhusishwa moja kwa moja na neno 'UHURU?' Hii inaweza kutafsiriwa kwa namna tofauti, pengine mtu wa ML si mpigania uhuru na hana mawazo ya kiukombozi licha ya mwanya wa ukombozi

kuwapo. Pia, mtu wa MC ametambua kuwapo kwa uhuru na anaonekana kuwa ni mpigania uhuru wa jamii yake.

Jambo la nne ni tafsiri ya picha kubwa ya mtu. Ni dhahiri kwamba binadamu huweza kuwasiliana kwa kutumia picha mbalimbali kwa sababu picha hizo hubeba ujumbe fulani (Pettersson, 2015). Jalada la MC lina picha kubwa ya mtu. Mtu huyo ameinua juu mikono yote miwili na ameshika mwenge katika mkono wake wa kulia. Uso wake una rangi nyeupe na anatazama juu. Pia, ameachama kinywa chake ishara ya kutangaza au kufurahia jambo fulani. Mambo haya yote yanaweza kuashiria kuwa huyu ni mtu ambaye ana uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii yake kwa sababu uhuru upo mikononi mwake. Nuru ameshaiona na ameamua kusimama na kutangaza mapambano. Aidha, mtu huyo amevaa mavazi (suti) yenye kuonesha kuwa pengine ni wa hadhi ya kati au ya juu. Mtu huyo amezungukwa na rangi ya njano, ishara kwamba kuna matumaini makubwa ya kupatikana kwa ukombozi dhidi ya adha ambazo watu wanakumbana nazo. Vilevile, katika picha hii linaonekana sikio moja tu la mtu huyo. Hali hii inaashiria kuwa hayuko njia panda ila ameshaamua kufanya jambo moja na anasikiliza upande mmoja tu, hachanganywi na mambo mengine. Nyuma yake kuna kundi la watu wanaomtazama. Sifa hizi zinamhusu mhusika Remi anayeonekana kuwa kiongozi na tegemeo la watu katika jamii yake. Hata hivyo, sifa hizi chanya za Remi zinajitokeza mwishoni kabisa.

Jalada la ML vilevile lina picha ya mtu lakini mtu huyu anaonekana kuwa tofauti na mtu aliyepo katika jalada la MC. Sura yake haionekani vizuri kwa kuwa rangi nyeusi imetawala. Kwa maoni yetu, hii ni ishara kuwa yupo katika matatizo. Sura hiyo imegawanyika katika sehemu kuu mbili: upande wenye rangi nyeusi zaidi licha ya rangi nyingine kuwapo na upande ambao una mchanganyiko wa rangi ya njano, nyeupe na nyeusi. Hii inaweza kuashiria kuwa mtu huyu yuko katika hali ya njia panda kimawazo. Uso wake unadhihirisha kwamba si mtu mwenye furaha kwa sababu ameukunja. Sura yake inaonesha masikio yote mawili. Hii inaweza kumaanisha kwamba mtu huyu bado anasikiliza pande mbili. Hivyo, bado haelewi afuate mambo ya upande upi. Kinywa chake kimefungwa, hii ni ishara ya mtu kukosa jambo la kusema hata kama angelitakiwa kusema. Pia, kutoonekana kwa mikono yake kunaweza kuashiria kwamba mtu huyu hana uwezo wa kufanya mambo kwa sababu hana mikono ya kufanyia, huku neno 'UHURU' likiwa pembeni yake. Hii inaweza kumaanisha kuwa hayuko huru licha ya kwamba yupo karibu na uhuru huo.

Aidha, nyuma yake hakuna watu wanaomtazama, hivyo huenda huyu si kiongozi. Mambo haya yanaonekana kumhusu Remi, hasa wakati bado hajaamua kurudi katika jamii yake na kuisaidia. Remi alikuwa njia panda kimawazo alipoanza


kuambiwa habari za kurudi nyumbani kwani alihitajika sehemu tatu: nyumbani ili amuoe Thoni (ikiwa tayari anaishi na Jane mjini), kanisani, pamoja na katika masuala ya kisiasa. Sifa hizi hasi za Remi zinajitokeza mwanzoni hadi katikati wakati katika MC picha inaonesha sifa chanya ambazo zimejitokeza mwishoni.


Jambo la tano ni tafsiri ya picha ya kundi la watu. Katika MC nyuma ya picha kubwa ya mtu kuna kundi la watu wanaomtazama mtu aliyeko mbele yao. Watu hao wana nyuso za rangi nyeupe. Wamezungukwa na rangi ya njano. Nyuso zao si za furaha licha ya kuonesha kuwa zina matumaini. Aidha, watu hao wanaonekana kuwa na matumaini na aliyeko mbele yao, ndiyo maana wanamtazama kwa makini kama kiongozi wao. Lakini, katika ML hakuna kundi la watu nyuma ya picha ya mtu. Hii inaashiria kuwa, huyu si kiongozi na hakuna anayemtegemea. Hali hii inakinzana na maudhui yaliyomo katika tamthiliya hii, ambapo licha ya Remi kuonekana kuwa na sifa ambazo si nzuri (mwanzoni), bado jamii yake haikukata tamaa. Hii ni kwa sababu iliendelea kumfuatilia na kumwona kama mtu pekee anayeweza kuwa kiongozi atakayewatatulia adha walizonazo.

Jambo la sita ni tafsiri ya picha ya nyumba. Katika jalada la MC hakuna picha ya nyumba lakini katika jalada la ML kuna picha ya nyumba. Nyumba hizo zipo nyuma ya picha ya mtu, kulia kwake. Nyumba hizo zinaonekana kuwa ndogondogo, za makuti, na zipo gizani. Aina hii ya nyumba inaashiria kuwa wakazi wa eneo husika wapo katika hali duni (maskini). Hata hivyo, picha hii haipo katika MC, hivyo ni jambo lililofanywa na mfasiri wa kazi hii.

Jambo la saba ni tafsiri ya rangi. Rangi huweza kubeba ujumbe kuhusu hisia, mawazo, na hali mbalimbali (Zammitto, 2005). Jalada la MC hiyo lina rangi ya njano, nyeusi na nyeupe. Rangi ya njano imetumika kwa kiasi kikubwa kuliko rangi nyingine. Rangi hutumiwa na waandishi kama mbinu ya usimbaji wa maana na ujumbe. Rangi huwakilisha maana mbalimbali. Rangi nyeusi katika kazi nyingi za Kiafrika huwakilisha Waafrika wenyewe pamoja na matatizo yao. Hivyo, hata picha kubwa ya mtu aliyeko mbele kabisa katika MC ambaye amevaa mavazi yenye rangi nyeusi inaashiria Uafrika wake. Rangi ya njano ni ishara ya mwangaza au matumaini aliyonayo mtu licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Rangi nyeupe inaonesha dalili za kupata au kuona suluhu ya matatizo mbalimbali. Katika ML, rangi nyeusi inaonekana kuwakilisha giza au hali ya umaskini. Ndiyo maana nyumba ndogondogo zinazoonekana kutokuwa na ubora zimezungukwa na rangi nyeusi. Aidha, rangi nyeusi katika picha ya mtu inaonesha kuwa mtu huyu ni Mwafrika. Pia, rangi ya njano na nyeupe zinaonesha kuwapo kwa nuru au tumaini la kukombolewa kwa watu licha ya matatizo mbalimbali yanayowakumba.

Vilevile, tathmini hii imefanywa katika tafsiri ya tamthiliya ya *Kifo Kisimani* iliyoandikwa na Kithaka wa Mberia (2001) kisha kutafsiriwa kama *Death at the Well* na Khalfan Kasu (2011). Katika tafsiri hii kuna mambo kadhaa ambayo yamejitokeza:




Jambo la kwanza ni tafsiri ya jina la kitabu. Jina la kitabu katika MC ni *Kifo Kisimani*. Katika ML ambayo ni ya lugha ya Kiingereza, jina hili limetafsiriwa kama *Death at the Well*. Kimsingi, tafsiri hii inaakisi maudhui yaliyomo ndani ya kazi husika. Hii ni kwa sababu hata katika tamthiliya husika, mhusika Mwelusi aliuliwa na Gege kisimani. Hivyo, hadhira lengwa wataweza kupata athari zinazowiana na hadhira chanzi.

Jambo la pili ni tafsiri ya picha ya mtu. Katika MC mbele kuna picha kubwa ya mtu. Mtu huyu uso wake unaonekana kutokuwa na furaha (anastaajabu jambo fulani). Mtu huyo ana sikio moja, jambo linaloweza kuashiria kuwa anasikiliza mawazo ya upande mmoja. Aidha, anaonekana sehemu ya kichwa tu bila mikono wala miguu. Suala hili linaweza kumaanisha kuwa mtu huyu licha ya kuyaona maovu bado hana uwezo wa kuyatatua. Katika ML, picha iliyoko mbele inaonesha mikono miwili ya binadamu iliyoshika nguzo ya seng`enge ikijaribu kuing`oa. Seng`enge hiyo ni kielelezo cha matatizo mbalimbali yanayowakumba wanajamii. Hivyo, mtu huyo (mhusika Mwelusi) anajaribu kuyatatua. Ikumbukwe kuwa, MC ina picha ya uso (kichwa) wa mtu pasipo mikono wala miguu wakati katika ML kuna picha ya mikono pekee. Jambo hili linaweza kusababisha kutofautiana kwa athari watakazopata hadhira chanzi na hadhira lengwa.

Jambo la tatu ni tafsiri ya picha ya watu wengi. Katika MC hakuna picha ya watu wengi katika jalada kama ilivyo katika ML. Pia, nyuma ya picha kubwa ya mikono ya mtu kuna picha ya kundi la watu walioinua mikono juu kana kwamba wanashangilia jambo. Pasi na shaka, wanashangilia jitihada za mikono miwili

inayoonekana kupata mafanikio katika kudondosha nguzo ya seng`enge inayowatenganisha watu hao na kisima. Jambo hili halijajitokeza katika MC. Hivyo, hali hiyo inaweza kusababisha kutofautiana kwa uelewekaji wa ujumbe wa matini husika kama ilivyo katika MC.

Jambo la nne ni tafsiri ya seng`enge. Katika MC hakuna uzio wowote uliooneshwa katika jalada la kitabu, ilhali katika ML kuna seng`enge. Seng`enge hii ni ishara ya utawala mbovu na wenye changamoto nyingi wa Mtemi Bokono. Pia, kuna picha ya mikono inayoonekana kujaribu kuondoa seng`enge hiyo, huku waya mmoja umekatika na watu wanashangilia. Watu hao wako nyuma ya seng`enge hiyo iliyowekwa kukizunguka kisima. Vitu hivi vyote havipo katika jalada la MC, ndiyo maana kuna uwezekano wa kutokuwapo kwa usawa wa athari za kiujumbe kati ya jalada la MC na ML.

Jambo la tano ni tafsiri ya rangi mbalimbali. Katika MC rangi kuu zinazoonekana zaidi ni rangi nyekundu, njano, na nyeusi. Jina la kitabu katika MC limeandikwa kwa rangi nyekundu. Mtu ameoneshwa akiwa na nywele nyeusi na uso pia ni mweusi. Rangi ya njano imejitokeza huku ikiwa na taswira ya matumaini waliyonayo watu juu ya changamoto walizonazo. Katika ML, baadhi ya rangi zinazojitokeza ni nyeupe, bluu, nyeusi, njano, na kahawia. Kwa jumla, rangi zilizotumika katika MC zimejitokeza pia katika ML. Hata hivyo, rangi ya bluu inayowakilisha maji (kisima) haipo katika MC, jambo linaloweza kusababisha tofauti za kiathari kwa walengwa. Katika ML rangi ya bluu ndiyo inayowakilisha taswira ya kisima.

Jambo la sita ni tafsiri ya picha ya kisima. Katika jalada la MC hakuna picha ya kisima lakini katika ML kuna picha ya kisima kilichozungushiwa seng`enge. Kuna picha ikionesha watu wakiwa nje ya seng`enge huku wakishangilia kuondoshwa kwa seng`enge hiyo. Hii ni ishara kuwa seng`enge hiyo inawazuia kufika upande wa pili wenye kisima. Utawala wa Mtemi Bokono uliwaruhusu watu kuteka maji siku tatu tu za wiki. Hivyo, wanaamua kupambana ili wapate haki ya kuteka maji kila wakihitaji. Hata hivyo, katika jalada la MC hakuna picha ya kisima.

Jambo la saba ni tafsiri ya picha ya mnazi. Katika jalada la MC kuna picha ya mti mithili ya mnazi. Hata hivyo, katika ML hakuna picha ya mnazi. Kwa kawaida minazi hustawi maeneo ya ukanda wa pwani. Hivyo, hadhira lengwa ikiona mnazi inaweza kupata ujumbe kuwa kazi husika ni ya mazingira ya pwani. Kwa hiyo, kutokuwapo kwa mnazi huo katika ML kunaweza kuathiri mandhari ya kazi husika sambamba na uelewekaji wa ujumbe uliokusudiwa.

**Matokeo ya Tathmini**

Kutokana na tathmini hii, imebainika kuwa kuna kushabihiana na kutofautiana kati ya vipengele vinavyounda jalada la MC na ML. Yafuatayo ni mambo yanayoshabihiana katika majalada ya tafsiri ya *Mtawa Mweusi* (*The Black Hermit*) na *Kifo Kisimani* (*Death at the Well*):

Mosi, kuna kufanana kwa matumizi ya rangi kati ya jalada la MC na jalada la ML, mathalani, rangi ya njano, nyeusi na rangi nyeupe. Pili, majalada yote yametumia picha za binadamu na vitu kama vile mwenge na nyumba. Mathalani, katika MC, *The Black Hermit*, kuna picha ya mtu akiwa ameshika mwenge huku akionekana kutangaza jambo fulani na nyuma yake kuna picha ya watu wanaomwangalia; kadhalika, katika ML, *Mtawa Mweusi*, kuna picha ya binadamu mbele kabisa ya jalada. Aidha, katika MC *Kifo Kisimani*, kuna picha ya mtu; vilevile katika ML, *Death at the Well*, kuna picha ya mikono ya mtu na watu wengi nyuma yake pamoja na seng`enge. Vitu hivi katika majalada haya vinalandana na maudhui ya matini husika. Jambo hili linasababisha kuwapo kwa ufanano wa kidhima kati ya MC na ML kama Nadharia ya Usawe wa Kidhima inavyoeleza.

Tatu, katika matini zote kuna maandishi mbalimbali yenye kusadifu maudhui ya matini husika. Katika tafsiri ya *Mtawa Mweusi*, jina *The Black Hermit* limetafsiriwa kama *Mtawa Mweusi*. Pia, picha ya mwenge iliyoko katika MC imetafsiriwa kwa maneno katika ML, yaani neno ‘UHURU’. Vilevile, jina *Kifo Kisimani* limetafsiriwa kama *Death at the Well*. Hivyo, kuna mfanano wa kiathari kati ya majalada ya MC (*The Black Hermit* na *Kifo Kisimani*) na majalada ya ML (*Mtawa Mweusi* na *Death at the Well*). Kwa hiyo, hata maudhui yake yanafanana na kusadifu yaliyomo katika kazi husika. Suala hili linasababisha kuwapo kwa uwiano wa kimaudhui kati ya MC na ML.

Licha ya kufanana huko, kuna vipengele vinavyotofautiana kati ya majalada ya MC (*The Black Hermit* na *Kifo Kisimani*) na ML (*Mtawa Mweusi* na *Death at the Well*). Zifuatazo ni hoja na kutofautiana huko:

Katika *The Black Hermit* (MC) kuna picha ya watu wengi nyuma ya picha kubwa ya mtu lakini katika ML hakuna picha ya watu wengi. Pia, picha ya mtu katika MC inaonekana kuwa na sikio moja wakati katika ML ina masikio mawili. Vilevile, katika ML kuna picha ya nyumba wakati katika jalada la MC haipo. Katika ML, nyumba hizo zinaonekana kuwa ndogondogo zikiwa katika giza. Aidha, katika ML kuna picha ya mtu anayeonekana kuwa na pande mbili zilizogawanywa kwa rangi.

Upande mmoja umetawaliwa na rangi nyeusi na upande mwingine kuna mchanganyiko wa rangi ya njano, nyeupe na nyeusi.

Katika *Kifo Kisimani* (MC) kuna picha ya mtu akionekana sehemu ya kichwa tu, na anaonekana kuwa na sikio moja wakati katika *Death at the Well* (ML) kuna picha kubwa ya mikono ya mtu na nyuma yake kuna picha ya watu wengi. Hivyo basi, tofauti hizi zinaweza kusababisha tofauti za kiuelewekaji wa ujumbe kwa hadhira lengwa. Jambo hili linaweza kusababisha kutofautiana kwa athari watakazopata hadhira chanzi na hadhira lengwa.

Hivyo basi, kufanana kwa tafsiri za vipengele vinavyounda MC na ML kunaweza kusababisha kuwiana kwa athari za MC kwa hadhira chanzi na athari za ML kwa hadhira lengwa. Kadhalika, kutofautiana kwa tafsiri ya vipengele vya MC na ML kunaweza kusababisha kutowiana kwa athari za ML kwa hadhira lengwa na athari za MC kwa hadhira chanzi. Ikumbukwe kuwa, Nadharia ya Usawe wa Kidhima inasisitiza kuwapo kwa ulinganifu kati ya athari za MC kwa hadhira chanzi na ML kwa hadhira lengwa.

**Mapendekezo**

Makala hii inapendekeza mambo kadhaa: Mosi, si lazima kila jalada la kitabu litafsiriwe, mengine yanaweza kuhamishwa kama yalivyo ili yasiathiri maana na ujumbe wa MC katika ML, hususani katika vipengele vya masilugha ambavyo mara nyingi hufahamika katika jamii nyingi.

Pili, vipengele vya masilugha kama vile rangi, michoro, alama na picha mbalimbali vitafsiriwe ikiwa vinaweza kueleweka tofauti kwa hadhira lengwa. Hata hivyo, umakini mkubwa na ubunifu wa hali ya juu usioathiri ujumbe wa MC unapaswa kutumika katika kuandaa jalada la ML.

Tatu, mpangilio wa vitu vinavyounda MC ni vyema uendane na ML. Mathalani, ikiwa MC jalada lake limeanza na jina la kitabu, jina la mwandishi na kisha picha mbalimbali, basi jalada la ML ni vyema likafuata mpangilio huo. Hii ni kwa sababu jambo lenye uzito ndilo huwekwa mwanzoni kwa kuwa huenda mwandishi ananuia kuwasilisha ujumbe fulani kupitia mpangilio husika.

Nne, malengo ya mwandaaji wa kazi ya tafsiri, malengo ya tafsiri yenyewe, na malengo ya mfasiri yasiwe na athari kubwa katika mchakato wa tafsiri ya jalada la kitabu kiasi cha kufanya majalada husika yalete athari tofauti. Hivyo, mfasiri anapaswa kuutumia uhuru alionao kwa umakini na kiutaalamu katika kutafsiri MC ili aweze kuzalisha ML yenye athari sawa na MC.

**Hitimisho**

Makala hii imetathmini tafsiri ya majalada ya vitabu katika tafsiri ya tamthiliya ya *Mtawa Mweusi* (*The Black Hermit*) na *Kifo Kisimani* (*Death at the Well*). Tathmini hii imezingatia zaidi suala la ulinganifu wa kidhima au kiathari kati ya MC na ML kama Nadharia ya Usawe wa Kidhima inavyosisitiza. Vipengele vilivyoshughulikiwa katika majalada ya tafsiri hizo ni vya lugha na masilugha. Hatimaye, makala imebaini kuwa kuna kushabihiana na kutofautiana kwa baadhi ya vipengele vya majalada ya MC na ML. Hivyo basi, wafasiri hawana budi kuwa makini na vipengele vinavyounda jalada la kitabu. Aidha, majalada ya tafsiri yaandaliwe kwa ubunifu kwa kuzingatia taarifa zilizomo katika MC. Hii ni kwa sababu jalada lililobuniwa vibaya linaashiria kuwa matini husika si nzuri kwa msomaji. Hata hivyo, si kila jalada lazima litafsiriwe, kwani linaweza kuhamishwa kama lilivyo na likaeleweka. Aidha, vipengele vya lugha vilivyomo katika jalada hilo vinaweza kutafsiriwa lakini vya masilugha vikaachwa ikiwa vinaeleweka kwa hadhira lengwa. Ikumbukwe kuwa, kadiri vipengele vya jalada la tafsiri vinavyofanana ndiyo husababisha kuendana kwa maudhui ya MC na ML na kadiri majalada hayo yanavyotofautiana ndivyo maana, ujumbe na athari za MC zitakavyotofautiana na ML.

**Marejeleo**

Benedicta, W. (2012). Personal Names and Identity in Literary Contexts. *Olso Studies in Language*, Juz. 4, Kur. 273-284.

Coker, M. (2014). *The Secrets to eBook Publishing Success: How to Reach More Readers with your Words.* Smashwords: Mark Coker.

Drew, N. & Sternberger, P. (2005). *By Its Cover: Modern American Book Cover Design*. Princeton: Architectural Press.

Kihore, Y.M. (2005). Uzingativu wa Sarufi katika Tafsiri. *Swahili Forum*, Juz. 12, Kur.109-120.

Lyons, S. (2017). To Judge a Book by Its Cover: A Genre Analysis about the Cover of a Book. *Grassroots Writting Research Journal*, Kur, 93-105.

Macaya, M. & Perea, M. (2014). Does Bold Emphasis Facilitate the Process of Visual-Word Recognition? *Spanish Journal of Psychology*, Juz. 17, Kur. 1-5.

Matkivska, N. (2014). Audiovisual Translation: Conception, Types, Characters' Speech and Translation Strategies Applied. *Kalbų Studijos*, Juz. 25, Kur. 38-44.

Mberia, K. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mberia, K. (2011). *Death at the Well.* Kimetafsiriwa na Kasu, K. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Mossop, B. (2018). Judging a Translation by Its Cover. *The Translator*, Juz. 24:1, Kur. 1-16.

Mwansoko, H.J.M., Mekacha, R.D.K., Masoko, D.L.W. & Mtesigwa, P.C.K. (2015). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

Nida, E. (1964). *Towards a Science of Traslating*. Leiden: E.J. Brill Press.

Pettersson, R. (2015). *Information Design: Image Design*. International Institute for Information design (III D).

Thiong`o, N. (1968). *The Black Hermit*. Nairobi, Kampala, Dar es Salaam, Kigali: East African Educational Publishers Ltd.

Thiong`o, N. (1970). *Mtawa Mweusi*. Kimetafsiriwa na Thiong`o, N. Nairobi, Kampala, Dar es Salaam: East African Educational Publishers Ltd.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Zammitto, V. (2005). The Expressions of Colours. *Proceedings of DiGRA 2005 Conference: Changing Views – Worlds in Play*, Juz. 3, Kur. 1-15.